

Huwenda umezunguka sana kwa watu kutafuta suruhisho la matatizo yako na huwenda hujapata majibu.

Leo nathubutu kukwambia kwamba kuna taarifa unapaswa uzifahamu kabla hujaendelea na safari ya kutafuta suruhisho la hayo matatizo yanayokusumbua.

Kitu muhimu zaidi ninachoweza kuthubutu kukwambia ni kwamba furaha, afya , ustawi, utajiri na mafanikio ya kila aina hivi vyote unastahili kuvipata na viro kwa ajili yako.

Unastahili kufanikiwa katika kila eneo unalotaka kufanikiwa.

Na habari njema zaidi ni kwamba mafanikio haya hayapomikononi mwa mtu yeeyeote wala hayako mbinguni ila yamo ndani yako.

Hivyo katika kitabu hiki nitakupa maarifa ya kukusaidia kuanza kuyaishi na kuyafaidi hayo mafanikio unayoyatamani kila siku.